

**HOTUBA YA MKURUGEZI MKUU WA TANTRADE KATIKA HAFLA  
YA KUFUNGA MAONESHU YA 46 YA BIASHARA YA KIMATAIFA  
YA DAR ES SALAAM, TAREHE 13 JULAI, 2022 KATIKA UWANJA  
WA MWL. J.K. NYERERE, BARABARA YA KILWA,  
DAR ES SALAAM**

*Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa  
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mgeni Rasmi;*

*Mheshimiwa Dkt. Ashatu K. Kijaji (Mb), Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na  
Biashara;*

*Mheshimiwa Omar Said Shaaban (MBW), Waziri wa Biashara na  
Maendeleo ya Viwanda, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;*

*Waheshimiwa Mawaziri wote mliopo hapa;*

*Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe (Mb.), Naibu Waziri wa  
Uwekezaji, Viwanda na Biashara;*

*Waheshimiwa Manaibu Waziri wote mlioko hapa;*

*Mheshimiwa Amos Makala, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;*

*Mheshimiwa Jokate Mwegelo, Mkuu wa Wilaya ya Temeke;*

*Prof. Godius Kayharara, Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji,  
Viwanda na Biashara;*

*Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu Mliopo hapa;*

*Waheshimiwa Mabalazi na Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa;*

*Mwenyekiti na makamu Mwenyekiti wa kamati ya Kudumu ya  
Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira;*

*Mwenyekiti na Wakurugenzi wa Bodi ya TanTrade;*

*Bi. Angelina Ngalula, Mwenyekiti na Mwakilishi wa Sekta Binafsi  
Tanzania;*

***Bi. Esther Mang'anya, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Azania na wadhamini wakuu wa Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam;***

***Viongozi wa Vyama vya Siasa na Dini Mliopo hapa;***

***Viongozi wa Mashirika ya Umma na Binafsi;***

***Menejimenti ya Wizara na ya TanTrade;***

***Ndugu Washiriki wa Maonesho;***

***Wageni Waalikwa;***

***Wanahabari;***

***Mabibi na Mabwana;***

***Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania***

### **Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Awali ya yote naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutukutanisha mahali hapa tukiwa na afya njema.

Pili kwa niaba ya Wafanyakazi wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), ninayo heshima kubwa kukushukuru wewe **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mgeni Rasmi** kwa kukubali mwaliko wetu na kushiriki pamoja nasi katika hafla hii ya ufungaji wa Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, 2022. Tumefarijika sana kukuona hapa. **Tunashukuru sana!**

Tatu, napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na Menejimenti ya Wizara kwa miongozo,

maelekezo na ushirikiano wao kabla na wakati wa Maonesho uliofanikisha Maonesho haya. Vilevile, napenda kumshukuru Mheshimiwa Omar Said Shaaban Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na Wizara yake kwa ushirikiano wao mkubwa wanaotupatia katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali. **Asanteni sana!**

Nne, natoa shukrani zangu za dhati kwa Viongozi wa Serikali wa Kitaifa, Viongozi wa Vyama vya Siasa na Dini pamoja na Viongozi wa Mashirika na Asasi mbalimbali, kwa kutenga muda wenu na kushiriki nasi katika hafla hii. Tunawashukuru pia wale wote walioweza kuyatembelea Maonesho haya kwa nyakati tofauti na kutoa maoni ili kuboresha zaidi kipindi kijacho. Hakika, ujio wenu umetupa faraja kubwa. Tumejiona hatuko peke yetu katika kuikuza Sekta hii ya Biashara na Maonesho nchini. **Tunawashukuru sana!**

Naishukuru pia Kamati Kuu ya Kitaifa ya Maandalizi, Kamati ya Ulinzi na Usalama na Kamati ya Afya kwa kazi kubwa waliyoifanya kufanikisha Maonesho haya.

Kwa kipekee kabisa nawashukuru Wadhamini na Wabia wetu mbalimbali waliojitoa kwa hali na mali kufanikisha Maonesho yetu wakiongozwa na Bi. Esther Mang'anya, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Azania ambao ni wadhamini wakuu wa Maonesho haya, MIC Tanzania – Tigo, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Wasafi Fm, Shirika la Bima la Taifa (NIC), Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Mamlaka ya Bima Tanzania (TIRA), Kinglion Investment Center, GiZ na

Group Six. Tunaomba muendeleo kujitoa katika programu zetu mbalimbali za ukuzaji biashara nchini ili kukuza na kuimarisha uchumi wetu.

Nawashukuru pia Wanahabari kutoka Vyombo mbalimbali vya Habari hapa nchini. Mmefanya kazi nzuri kuuhabarisha Umma juu ya uwepo wa Maonesho haya na fursa mbalimbali zinazopatikana katika Maonesho haya. **Asanteni sana !**

Mwisho lakini si kwa umuhimu, nawashukuru Washiriki na Watembelaji wote wa Maonesho ambao kwakweli bila ninyi, tusingesherehekea Mafanikio tuliyo nayo hivi leo. **Asanteni sana na karibu tena na tena.**

### **Mheshimiwa Mgeni Rasmi**

Kauli Mbiu ya maonesho haya ni “**Tanzania:Mahali sahihi pa Biashara na Uwekezaji**” ikilenga kuunga mkono juhudi za **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, katika kukuza mahusiano ya kidiplomasia na kiuchumi hususan katika kuchochea Uwekezaji na Biashara.

### **Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Maonesho ya mwaka huu yalikuwa na utofauti ukilinganisha na Maonesho mengine kutokana na uwepo wa vionjo tofauti vikiwemo Programu ya *Watoto wetu Urithi wetu* ambapo jumla ya wanafunzi 87 wa shule za Sekondari kutoka maeneo mbalimbali yakiwemo Kaskazini B unguja, Pemba, Babati, Luangwa, Bahi na Dar es Salaam walitembelea Maonesho haya. Wanafunzi hawa wamejifunza kwa vitendo juu ya Ujasiriamali, kuyatambua majukumu ya Taasisi za Serikali na kupata

ufahamu wa mambo mbalimbali kutoka Mataifa yaliyoshiriki Maonesho haya. Vilevile walitembelea vivutio mbalimbali vilivyoko katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Pia kulikuwa na Mikutano ya Wafanyabiashara ya Ana kwa Ana kwa Wawekezaji, Wanunuzi na Wauzaji wa ndani na nje ya nchi (Investors, Buyers and Sellers meeting) ambapo wadau 284 wanaojumuisha wazalishaji wa ndani ya nchi na wanunuzi katika Sekta za Madini, Viwanda, Vifaa vya Ujenzi, Kilimo, Uchumi wa Buluu, vifaa tiba na dawa za binadamu walishiriki. Katika mikutano hiyo, majadiliano yaliyohusisha mauzo ya bidhaa zenye thamani ya shilingi **Bilioni Mia Tisa Sitini na Tisa, Mia Sita Thelathini Elfu na Laki Nane** (969,630,800,000/-) na ya Uwekezaji yenye thamani ya shilingi **Bilioni kumi** (10,000,000,000/-) yalifanyika.

Vilevile ushirikiano baina ya TanTrade na Wakala wa Mabasi yaendayo haraka (DART) kwa uanzishwaji wa njia mpya za usafiri kutoka kituo cha DART Gerezani na Mbagala kuja katika viwanja vya Saba Saba uliwezesha watembeleaji kufika kirahisi katika Maonesho haya na hivyo kuongeza idadi ya watembeleaji.

### **Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kutokana na kuwa Maonesho haya ni ya Kimataifa, tumeshirikiana na wadau mbalimbali na kuwatengea siku maalumu katika kutangaza tamaduni pamoja kazi au huduma wanazozitoa, zikiwemo Siku ya Kitaifa ya Iran, Maadhimisho ya miaka 41 ya SUMA J.K.T, siku ya Utamaduni wa Zanzibar, siku ya Ushirika, Siku ya Waokaji, Siku ya Posta na Siku

ya Kongani ya Batiki. Vilevile, wasanii walipata fursa ya kuonesha kazi zao kupitia jukwaa la *Meet your Star* ilioratibiwa na Zamaradi Mketema pamoja na jukwaa la *Wasafi Village* lilioratibiwa na **Wasafi Media**. Hivyo, niwapongeze sana wadau wetu hawa kwa kufanikisha shughuli hizi na kufanya Maonesho haya yaletе tija kwa watembeleaji na Washiriki kwa ujumla.

### **Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Katika Maonesho haya tumepata mafanikio mbalimbali ikiwemo ongezeko la ushiriki kutoka Kampuni 3,002 mwaka 2021 na kufikia Kampuni **3,425** mwaka huu ambapo kati yake Kampuni **3,200** ni za washiriki wa ndani na Kampuni **225** ni washiriki kutoka Nchi **23** zikiwemo Misri, China, India, Indonesia, Korea Kusini, Kenya, Rwanda, Ghana, Marekani, Pakistani, Burundi, Singapore, Vietnam, Uganda, Nigeria, Urusi, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Iran, Thailand, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Ujerumani, Botswana na Syria. Hakika ni mafanikio makubwa. Licha ya uwepo wa Ugonjwa wa Virusi vya Korona (UVIKO-19) unaoendelea kuikumba Dunia, lakini wenzetu hawa wametuunga mkono. **Tunawashukuru sana !**

### **Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Ninapomalizia nipende kukuhakikishia wewe pamoja na Wadau wote wa Sekta ya Biashara kwa ujumla kuwa, tutaendelea kusimamia vyema Taasisi hii ili kuhakikisha Sekta ya Biashara nchini inaendelea kutoa mchango katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. Vilevile, tutaendelea kusimamia na kuyaboresha zaidi Maonesho haya ili yawe na tija stahiki

katika kupata masoko ya bidhaa na huduma mbalimbali hususan zile zinazozalishwa hapa nchini.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Baada ya kusema hayo, naomba sasa nirudishe kipaza sauti kwa Mshereheshaji ili aweze kuendelea na program zinazofuata.

**Nawashukuru sana kwa kunisikiliza!**